## UENEZAJI WA VIRUSI VYA UKIMWI KWA KUFANYA MAPENZI
## NA ELEANOR TURNBULL

Virusi vya ukimwi hupatikana kwenye damu na maji maji yoyote ya mwili. Virusi hivi huumiza CD4 ambayo hupatikana kwenye damu na pia husaidia kukinga mwili. virusi vya ukimwi huumiza CD4 na huimaliza nguvu na kwasababu hii mwili huisha nguvu na mgonjwa hushikwa na magonjwa tofauti haraka na mwishowe kushikwa n augonjwa wa ukimwi. Njia moja ya kupitisha virusi vya ukimwi ni kufanya mapenzi bila kujikinga kwa mfano kwa kutumia kondomu. Watu ambao wana uhatari wa kuwa na virusi vya ukimwi ni wale wako na zaidi ya mpenzi mmoja na pia kama anajihusisha na ukahaba au kutumia madawa ya kulevya ya kujidunga.Kuwa na mpenzi mmoja ndio njia mmoja muhimiu ya kujikinga dhidi ya ukimwi.

### UPISHAJI WA VIRUSI VYA UKIMWI WAKATI WA KUFANYA MAPENZI

Virusi vya ukimwi hupitishwa kwa njia ya majimaji ya mwili yanao kuwa kwa mwanamume na pia mwanamke wakati wa kufanya mapenzi . virusi hivi hupitishwa wakati maji maji haya ya mwili yanapatana na damu kwa mfano mtu akifanya mapenzi bila kutumia kondomu na mwanamke ana kidonda kidogo ambacho hakionekani basi maji maji yenye virusi hupita na kuingia kwenye damu yake pia mwanamume anaweza kuwa na kidonda kidogo ambacho hakionekani na basi wana shikishwa virusi vya ukimwi. Pia hatari nyingine ni kufanya mapenzi na mwanamke ambaye ako na damu yake ya mwezi hii uongeza hatari ya kushikishana virusi vya ukimwi.

Wakati mwanamke ana fanya mapenzi bila kutumia kondomu hatari ni kubwa kuliko mwanamume kwani pande za siri za mwanamke ni kubwa.Pia njia za utamaduni kama kutahirisha wanawake zinawaweka kwa hatari kwani makali yanaweza kuwa si safi au zina virusi vya ukimwi pia kama ametahiriwa na bado hajapona vizuri na akawa na kidonda na kufanya mapenzi na mtu ambaye ana virusi vya ukimwi basi ni rahisi sana kusambaziwa virusi.

Mwanamke ana weza kuwa na ugonjwa ya zinaa na ugonjwa huu una weza leta vidonda ambazo virusi vya ukimwi vina weza pita akifanya mapenzi bila kutumia kondomu.

Wasichana wadogo pia wana hatari ya kupata virusi ya ukimwi wakifanya mapenzi bila kutumia kondomu kwani misuli yao haijakoma na inaweza kupasuka au kuumizwa. Pia mwanamke akilazimishwa kufanya mapenzi kwa nguvu virusi vina weza kupita kwani kunaweza kuwa na vidonda.

### UPISHAJI WA VIRUSI VYA UKIMWI WAKATI WA KUFANYA MAPENZI KWA NJIA NYINGINE

Kufanya mapenzi bila kutumia kondomu kati ya wanaume wawili au mwanamke na mwanamume kwa kutumia njia zingine iko na hatari kubwa kuliko njia ya kawaida ya kufanya mapenzi. Ngozi haina nguvu na kwa hivyo kuna hatari kubwa ya kwamba ina weza umia wakati wa kufanya mapenzi na virusi vya ukimwi kupita n akuingia kwenye damu.

**UPISHAJI WA VIRUSI VYA UKIMWI WAKATI WA KUFANYA MAPENZI KWA NJIA NYINGINE YA KUTUMIA MDOMO**

Hatari ya kupitisha virusi kwa njia hii si kubwa sana kama njia hizo zingine lakini virusi vinaweza ambukizwa. Mdomo unaweza kuwa na kidonda na kwa hivyo virusi vinaweza enezwa kwa kutumia njia hii na hatari iko juu kama mtu huyo ana vidonda kwa mdomo lakini hii ina weza kuchungwa kwa kutumia kondomu kwa mwanamume na pia mwanamke.

**HATARI YA WANAWAKE KUPATA VIRUSI VYA UKIMWI.**

Wanawake wako katika hatari ya kuwa virusi vya ukimwi ki jamii, kimwili na kwasababu ya shida ya pesa. Ukimwi unaweza zuiwa kwa kutumia kondomu ,kupimwa ugonjwa za zinaa na kuenda hospitali mara kwa mara.
Kwa upande wa ki jamii ni ngumu kuzuia ugonjwa huu kuenea kwani mwanamke ana fuata kile anacho ambiwa na mumewe, kwanza mwanamume anaweza oa wanawake wengi na pia kutafuta Malaya. Pia wanawake wanaogopa kuachwa bila pesa au kunyanganywa watoto wao kwa hivyo wana vumilia na kukaa na wanaume hao na kwasababu wako katika hatari ya kuambukizwa virusi vya ukimwi
Pia ukosaji wa pesa una sababisha wanawake kuwa makahaba na mara nyingi hawatumi kondomu na wateja wao kama wanapatiwa pesa zaidi na hii inahatarisha maisha yao.

## Njia za kujichunga

### Kondomu

Kondomu zikitumiwa vizuri husaidia katika ueneaji wa virusi vya ukimwi kwani kondomu huzuia maji maji ya mwanamume kutoka na pia huzuia ugonjwa za zinaa. Pia huzuia magonjwa ya zinaa kwani maji maji za mwili haya patani. kondomu husaidia katika kukomesha virusi vya ukimwi kuenea na pia magonjwa ya zinaa. Ziki tumiwa virusi kondomu hufanya kazi lakini haina uhakika kabisa katika kuzuia magonjwa haya pamoja na virusi vya ukimwi.

### Uponyaji wa magonjwa ya zinaa.

Magonjwa ya zinaa huongeza hatari ya uenezaji wa virusi vya ukimwi. Utumiaji wa kondomu ni muhimu kwani husaidia maji maji ya mwili ya si patane na pia kama mtu ako na kidonda basi maji maji na damu hayapatani , pia kuenda hospitali kuangaliwa mara kwa mara ni muhimu sana kama mtu ako na zaidi ya mpenzi mmoja ama ni kahaba.

## Kutahirishwa

Kutahirishwa kwa mwananmume hupunguza hatari ya kupatwa na virusi vya ukimwi ,kama ngozi haijatolewa virusi vinaweza kuishi kwa muda mrefu kwani kuna joto na virusi vinaishi kwa muda mrefu na hii inaongeeza hatari.
Kuna wasiwasi kwani wanaume wanaamni mtu akitahirishwa hawezi kuambukizwa virusi na kwasababu hii wana zaidi ya mpenzi mmoja. Pia wana wacha kutumia kondomu ambaye inauhakika wa asilimia themanini (80%) na kutahirishwa ina uhakika wa asilimia hamsini (50%) .
Wanaume ambao hawa jatahirishwa vizuri wako katika hatari kwani kutumia makali ambayo si safi ina weza eneza virusi vya ukimwi. Pia kidonda isipo pona vizuri pia inaongeza hatari ya kupata virusi. Kutahirishwa kwa wanaume ina weza kusaidia wanaume wakati inafanyiwa mahali pasafi na kwa kutumia njia inayo paswa.

## Mwishowe

Ueneaji wa virusi vya ukimwi kwa kufanya mapenzi uko chini ikilinganishwa na magonjwa mengine ya zinaa lakini virusi vya ukimwi ni hatari na huleta ugonjwa wa ukimwi na kwa hivyo inapaswa kuchungwa na kuzuiwa.
Kondomu isipo valiwa wakati wa kufanya mapenzi kwa njia yoyote basi kuna hatari ya kueneza virusi vya ukimwi.
Hatari inaongezeka wakati mtu anafanya mapenzi bila kutumia kondomu na mtu ambaye ana zaidi ya mpenzi mmoja kama vile makahaba ama mtu ambaye anatumia madawa ya kulevya ya kujidunga.
Mwishowe magonjwa yote ya zinaa yanapaswa kutibiwa na mtu kufuata maagizo ya daktari.